**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU KATOKE
S. L. P. 1178, BUKOBA.
Barua pepe: katoketc@moe.go.tz
katoketc@gmail.com
+255 763 815205, +255 755 239857

Kumb.Na: CCU/KAT/JOIN/…..

11/06/2026.

Bwana/Bibi/Bi...................................

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI 2026/2027.**

## 1. UTANGULIZI

Tunayo furaha kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada Elimu ya Awali katika Chuo cha Ualimu Katoke kama mwanachuo wa bweni/masafa

## 2. MAHALI CHUO KILIPO:

Chuo cha Ualimu Katoke kipo Mkoani Kagera, Wilaya ya Muleba umbali wa Km: 50 kutoka Bukoba Mjini, ukifuata barabara iendayo Biharamulo; vilevile Km: 23 kutoka Muleba ukifuata barabara ya Biharamulo kuelekea Bukoba Mjini. Ukitokea Mwanza au Bihararnulo kwa barabara, utafika kwanza Muleba kisha Katoke. Barabara hii hupitia katika eneo Ia chuo kiasi cha Mita 300 kutoka kwenye majengo ya Chuo. Kama ni m chana, ni rahisi kupambanua kwani kibao kilichoandikwa '**Chuo Cha Ualimu Katoke',** kipo barabarani. Ukifika unaongozwa na barabara yenye miti mirefu pande zote. **Ni karibu, usidanganywe na waendesha pikipiki.**

**DIRA YA CHUO:**
Kuwa na Mwalimu Mweledi, anayemudu Mazingira, mwenye fikra za Kiutandawazi na Nidhamu, anayekuza Utamaduni wa Taifa kwa Mtoto.
**MOTO YA CHUO:** "Nakaza Mwendo"

## 3.MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

### A. VYETI NA VITAMBULISHO:

Ili kuthibitisha kuwa wewe ndiye uliyechaguliwa kujiunga na chuo hiki, LAZIMA uje na vitu vifuatavyo:-

(i) Cheti halisi cha matokeo ya Mtihani/Mitihani (National form vi/GATCE Certificate) au Result Slip halisi kwa wale waliohitimu Mwaka 2026.
(ii) Cheti cha shule/Chuo kinachoonesha kuhitimu katika shule husika (school leaving certificate)/chenye picha/ saini na muhuri wa mkuu wa shule .
(iii) Cheti cha mganga anayetambuliwa na serikali kuthibitisha afya yako. Fomu hiyo imeambatishwa. **KIAMBATISHO NA. 1**
(iv) Barua ya Chuo inayokuita kujiunga na chuo hiki. (Joining Instructions)
(v) Cheti halisi cha kuzaliwa.
(vi) Paspoti size mbili.

NB: **Vyote hapo juu ni mubimu sana kuja navyo chuoni.**

## B. ADA:

Kila mwanachuo atatakiwa kulipa **ADA Tsh. 450,000/=** (mia nne hamsini elfu) kwa mwaka, kwa ajili ya kugharimia mafunzo.Unaweza kulipa **Tsh. 225,000/=** (Mia mbili ishirini na tano Elfu) mwanzoni mwa kila muhula. Unasisitizwa kulipa ADA inayotakiwa.

Fedha ya ADA hulipwa kwa kutumia namba ya utambulisho ya mlipaji (Control number). Tafadhali wasiliana na mhasibu wa chuo kwa simu **namba 0763053890** ili akupatie control number utakayotumia kulipa ada tu.
**NB.Kila mwanachuo aliyechaguliwa anatakiwa kuja na stakabadhi ya malipo ya ada. Jitahidi kulipia benki kwa control number uliyopewa na mhasibu.**

## C. MICHANGO

a) MICHANGO KWA WALIMU TARAJALI

Michango mingine ambayo hutolewa chuoni huwekwa kwenye akaunti ya chuo, Benki ya **NMB- KATOKE TEACHERS' COLLEGE DEVELOPMENT FUND** - ACCOUNT **NO: 3200 110 00 03. Jitahidi kulipia benki kwa akaunti uliyopewa hapo juu. Michango hiyo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-**

| **Aina ya Mchango** | **Kiasi katika shilingi za Tanzania na muda** |
|---|---|
| Usajili | **20,000/= kwa mwaka.** |
| Ulinzi | **30,000/= kw a mwaka** |
| Usafi na mazingira | **20,000/= kwa mwaka** |
| Michezo | **30,000/= kwa mwaka** |
| Serikali ya wanachuo | **5,000/= kwa mwaka** |
| Huduma ya kwanza | **10,000/= kwa mwaka** |
| Ukarabati | **25,000/= kwa mwaka** |

**NB: Ada ya mtihani wa Taifa hulipwa mwanzo mwa muhula wa kwanza mwaka wa pili kulingana na maelekezo ya Baraza la Miyihani la Tanzania kwa wakati huo.**
Aidha, kila mwanachuo anatakiwa kuwa na fedha za matumizi binafsi kwa ajili ya mahitaji yake madogomadogo awapo chuoni.

b) MICHANGO KWA NJIA YA MASAFA KWA WALIMU KAZINI

Michango hii hutolewa chuoni na kuwekwa kwenye akaunti ya Chuo kama inanavyoonekana kwenye kipengele C (a) hapo juu na michango hiyo imeanishwa kwenye jedwali lifuatalo

| **Aina ya Mchango** | **Kiasi katika shilingi za Tanzania na muda** |
|---|---|
| Usajili | **20,000/= kwa mwaka** |
| Huduma ya kwanza | **10,000/= kw a mwaka** |
| Serikali ya wanachuo | **5,000/= kwa mwaka** |
| Ufuatiliaji na uendeshaji wa mafunzo | **40,000/= kwa mwaka** |
| Ukarabati | **25,000/= kwa mwaka** |
| Michezo | **30,000/= kwa mwaka** |
| Usafin a mazingira | **20,000/= kwa mwaka** |
| **JUMLA** | **150,000/= kwa mwaka** |

**NB: Ada ya mtihani wa Taifa hulipwa mwanzo mwa muhula wa kwanza mwaka wa pili kulingana na maelekezo ya Baraza la Miyihani la Tanzania kwa wakati huo.**

## D. KADI YA NHIF:

**Kama huna kadi ya NHIF unatakiwa kuja na pesa taslimu Tsh. 50,400/= kwa ajili ya kulipia bima ya afya (NHIF) . NI LAZIMA KULIPA BIMA YA AFYA KWA YULE AMBAYE HANA KADI YA BIMA YA AFYA.**

## E. MAVAZI KWA WALIMU TARAJALI.


a) SARE KWA WANAUME

i. Suruali ya buluu nyeusi (dark blue ***angalia picha 1.1***) na nyeusi yenye marinda mawili yenye mkunjo chini (turn up ***angalia picha 1.2***). Suruali nyeusi itavaliwa siku za Jumatatu hadi Jumatano na suruali ya buluu nyeusi itavaliwa siku za Alhamisi na Ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na suruali linaweza kuvaliwa. Suruali itavaliwa na mkanda mweusi.
ii. Shati liwe buluu bahari (light blue) mikono mirefu.
iii. Tai ndefu buluu nyeusi (dark blue) au nyeusi. Tai itavaliwa kuendana na rangi ya suruali. Angalia picha 1.1

**Picha 1.1**
*Rangi ya Suruali, shati na tai kwa buluu nyeusi*



**Picha 1.2**
*Suruali ya mfano*



iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza (kufunika) kisigino kifupi. Viatu vitavaliwa na soksi ndefu nyeusi. Hairuhusiwi kuvalia suruali chini ya kiuno ( mlegezo).
v. Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe, 'track suit' ya buluu bahari, raba na soksi za michezo (bluu/nyeusi zenye fito nyeupe. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.
vi. Katoke mara nyingi kuna mvua nyingi, uje na mwavuli na viatu vya mvua.
vii. Uje na reki yenye mpini moja na fyekeo /kotama.
viii. Uvaaji wa jinzi, kaptula, bangili, cheni, vimodo, skafu, makobazi, vilaka, na pete (zisizo za ndoa) na vingine vinavyofanana na hivyo hauruhusiwi.

b) SARE KWA WANAWAKE.

i. Sketi rinda boksi(***Angalia picha 1.4***) ya buluu nyeusi (dark blue) na nyeusi zenye urefu unaozidi magoti na zisizobana. Sketi nyeusi itavaliwa siku za Jumatatu hadi Jumatano na sketi ya buluu


nyeusi itavaliwa siku za Alhamisi na Ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na rangi ya sketi linaweza kuvaliwa.

ii. Shati liwe 'light blue' mikono mirefu na tai ndefu 'dark blue' au nyeusi. Tai iendane na rangi ya sketi. Angalia picha 1.3.

**Picha 1.3**
*Rangi ya Sketi, shati na tai kwa buluu nyeusi*



**Picha 1.4**
*Sketi ya mfano*



iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza kisigino kifupi, soksi ndefu nyeupe.

iv. Nywele zichanwe au zisukwe mtindo wa roda (twende kilioni) mistari mitano (5) hadi nane (8) au kubanwa kisogoni kwa kibanio cheusi.

v. Mwanachuo atakayependa kujistili kwa vazi la hijab, liwe la rangi ya light blue(isitofautiane na rangi ya shati)

vi. Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe, 'track suit' ya buluu bahari, raba na soksi za michezo (bluu/nyeusi zenye fito nyeupe. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.

vii. Katoke mara nyingi kuna mvua nyingi, uje na mwavuli na viatu vya mvua.

viii. Uje na jembe yenye mpini 1.

ix. Uvaaji wa nguo angavu, khanga, kitenge, kofia, kilemba, hereni, bangili, mkufu, shanga, pensi, sketi fupi, nguo zenye mpasuo unaozidi magoti, makobazi na pete ( isipokuwa pete ya ndoa) hauruhusiwi.

c) MAVAZI MENGINE MUHIMU

Uje na nguo chache ambazo si sare ya chuo zenye hadhi ya kiualimu, ambazo utavaa ukiwa chuoni muda ambao hautakuwa wa darasani. Aidha, nguo hizo zitatumika pia katika shughuli za kuabudu kulingana na imani yako.

## F. MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI:

i. Gharama ya kukodisha godoro ni Tshs. I0,000/= kwa mwaka kwa wale watakaowahi na fedha hii inawekwa katika akaunti ya Michango ya chuo, au waweza kuja na godoro lako lenye vipimo inchi 2.5xfuti 6 kwa kuwa magodoro yaliyopo chuoni ni machache.

ii. Uje na shuka mbili (2) za rangi ya pink, blanketi, mto na foronya za pink kwa wasichana.

iii. Uje na shuka mbili(2) za rangi ya bluu ,blanketi na foronya za bluu kwa wavulana

iv. Neti nyeupe yenye pembe nne

## G. MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA TAALUMA:

Uje na madaftari ya kutosha yasiyopungua 14 makubwa; mathematical set, kalamu na penseli za kutosha ; rimu 1 ya karatasi A4 na Kibao tobo na karatasi zake zizopungua 20 kwa ajili ya umahiri wa lugha ya alama(LAT).

## 3. AFYA YA MWANACHUO:

Mwanachuo aliyechaguliwa atatakiwa kupimwa kuthibitisha afya yake. FOMU kwa ajili ya kupima afya imeonyeshwa katika **KIAMBATISHO NA. 1.** Matibabu hutolewa kwa magonjwa kama taratibu za NHIF zinavyoelekeza. Uwapo chuoni utapewa sehemu ya kulala, kitanda na chakula, lakini chuo hakitoi chakula maalum (" special diet" wala " light diet"). Uje na sahani moja, bakuli moja, kikombe kimoja visivyokuwa vya plastic na kijiko kimoja kwa ajili ya chakula. Unatakiwa uje na ndoo ya lita 20 na mfagio mmoja wa chelewa kwa ajili ya usafi

## 4.TARATIBU ZA CHUO:

Ufikapo chuoni, Mratibu wa Masuala ya Wanachuo atakupa maelekezo ya namna ya kuishi chuoni. Utapewa nakala inayoonesha Kanuni na taratibu za chuo na fomu ya kujaza kukiri kufuata taratibu zote uwapo chuoni. Kwa kifupi utatakiwa uwe **"MWAMINIFU, MTIIFU NA MWENYE NIDHAMU YA HALI YA JUU"** muda wote utakaokuwa hapa chuoni. Unakuja kujifunza ili uwe mwalimu bora unatakiwa kuweka juhudi katika masomo. Ukwepaji wa vipindi **hauruhusiwi,** utalazimika kuzingatia ratiba ya chuo. Aidha, kila mwanachuo atakuwa na uhuru wa kuabudu kwa dini na dhehebu lake.

MWISHO:
Tunakukaribisha sana Chuo cha Ualimu Katoke, kwa matumaini kuwa utakuwa mwanachuo mwema, hodari, unayejiheshimu na kuwaheshimu wengine kwa mwenendo wako jumuiya nzima ya chuo ifurahie kuwepo kwako hapa chuoni. Chuo kitafunguliwa rasmi 17/08/2026 . Hivyo, unashauriwa kuwahi.

Tunakutakia Safari Njema.

**KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU KATOKE**

Michael F. Ntwale
MKUU WA CHUO.
CHUO CHA UALIMU KATOKE
S. L. P. *1178*
BUKOBA

**KIAMBATISHO NA. 1**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

TO: The Medical Officer

From: ............................ .

..............................................

.......................................... ·..

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full timeteachers course.

A: I. (a) Eye - sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(t) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.
B: Blood Group

Date: ……… .. ... ... .... ... ..

Signature .. ... . ... .. . .. . ... ... ..... ... .

Official Stamp